



Maswali na Majibu (VCT)

Q. VCT ni nini?

VCT ni jina ya kizungu ambayo inamaanisha kufundishwa na kupimwa virusi vya ukimwi, kwa kujitolelea.

Q. Kupimwa virusi vya ukimwi ni nini?

Unaweza kupimwa virusi vya ukimwi kwa kutumia damu, damu kidogo inachukuliwa na inapimwa kwenye kliniki za VCT ambazo pia huongelesha watu juu ya virusi vya ukimwi na pia njia za kujikinga. Hospitali mingi hufanya upimaji wa virusi vya ukimwi. Kwasababu watu wa jamaa moja wanaweza dharau mtu ambaye anaenda kupimwa virusi, mtu anaweza kwenda kupimwa kwa hospitali za mbali ambapo hajulikani.

Q. Kupimwa kwa siri ni nini?

Hii inamaanisha yakwamba ni wewe pekee yako na yule anayefanya kipimo hicho mutajuwa hali yako, pia matokeo hayataonesha jina yako na utapatiwa nambari ambayo itatumiwa badala ya jina yako.

Q. Ni vipimo gani zinaonesha jina?

Hizi vipimo zinaitwa Nominal (kwa kimombo) lakini kabla ya kupimwa unaweza kuuliza maswali kama (1) ni lazima ni peane jina yangu?(2) Matokeo yatawekwa kwa utafiti ili watu wengine waweze kuona?

Q. Nini itafanyika nikienda kupimwa?

Kwanza ni lazima mtu kupewa mawaidha, hii ni siri na unapewa nafasi ya kuuliza maswali juu ya kupimwa. Mahali mingi ya kupimwa ni lazima kupeana ruhusa ya kupimwa na unapaswa kuweka sahihi. Damu kidogo inachukuliwa na kupimwa (kuna vipimo za haraka na pia kuna zingine ambazo huchukua muda) watapima na ikionyesha mwili hauna virusi basi inamaanisha uko sawa lakini ikionyesha yakwamba ina virusi basi watachukua damu tena na kupima ili kuhakikisha, mtu yeyote anayepimwa ni lazima apewe mawaidha baada ya kupimwa.

Q. Nafasi ya kuambukizwa virusi na kupata virusi inamaanisha nini?

Mtu akiambukizwa virusi na apate virusi hivi kuna nafasi ambayo akipimwa damu haitaonesha virusi. Kwa mfano mtu akiambukizwa virusi leo halafu apimwe siku y pili matokea yataonyesha mtu hana virusi, nafasi hii huwa kwa muda wa wiki mbili hadi miezi tatu. Watu wakupeana mawaidha hueleza mtu yeyote ambaye anapimwa ajipime tena baada ya miezi mitatu kwani anaweza kuwa katika nafasi hii ambayo kwa lugha ya kiingereza inaitwa window period.